№216

DAWASA YETU

WIKI HII - TOLEO NA: 0216 TAREHE: 1.9.2025 HADI 7.9.2025

# DC MSANDO ARIDHISHWA UZALISHAJI MAJI RUVU JUU, ATOA MAAGIZO DAWASA





Mkuu wa Wilaya ya Ubungo (DC), Mheshimiwa **Albert Msando** amefanya ziara katika mtambo wa uzalishaji maji **Ruvu Juu** kwa lengo la kuona na kujiridhisha hali ya uzalishaji wa maji katika mtambo huo ambao unahudumia sehemu kubwa ya **Wilaya ya Ubungo**.

Katika ziara yake hiyo aliyoambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama **Wilaya ya Ubungo** pamoja na watendaji wa **DAWASA**, **DC Msando** ameridhishwa na hali ya uzalishaji maji huku akitoa maagizo kwa **DAWASA** kutatua changamoto zilizopo kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji.

"Tumefika hapa **Ruvu Juu** na tumejiridhisha uzalishaji wa maji upo vizuri, tunafahamu kulikuwa na matengenezo yanaendelea na kusababisha baadhi ya maeneo kukosa maji tumeona matengenezo yamekamilika na huduma inarejea kwa wananchi," amesema **Msando.**

Msando ametoa maagizo kwa watendaji wa **DAWASA** hasa waliopo **Wilaya ya Ubungo** kuhakikisha maji yanayozalishwa yanawafikia wananchi bila kikwazo na kutoa taarifa kwa wakati pale panapotokea changamoto yeyote ya huduma lakini zaidi wanaopata maji kwa migao wajue siku gani wanapata na ratiba hiyo isimamiwe bila kupindishwa.

"Nirudie kusema tena, swala la upotevu wa maji halikubaliki, Serikali inatumia gharama kubwa kuchakata maji haya mpaka yanapomfikia mteja uwekezaji huu lazima uthaminiwe na tusimamie vyema kila mwananchi apate maji," amesema **Msando**.

Meneja wa Mtambo wa uzalishaji maji **Ruvu Juu**, Mhandisi **Juma Kasekwa** amesema kwasasa hali ya uzalishaji imerejea katika hali ya kawaida na maeneo yaliyokuwa hayapati maji, huduma inaendelea kuimarika.

"Katika hali ya kuboresha uzalishaji maji katika mtambo wetu wa **Ruvu Juu**, Serikali imetupatia zaidi ya **Shilingi bilioni 1** kununua pampu mbili mpya ambazo ni mategemeo yetu mpaka ifikapo **mwezi Novemba** tutakua tumezifunga na Kuongeza uzalishaji wa maji," amesema **Kasekwa**.